



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUMBULI



FEBRUARY 21, 2023

**TANGAZO LA KAZI YA UJENZI KWA AJILI YA UJENZI WA
JENGO LA MAONESHU YA NANENANE-MOROGORO
AWAMU YA KWANZA**

(LGA/164/2022/2023/FA/W/01)

Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya ya Bumbuli anatangaza nafasi ya kazi ya ujenzi wa Jenngo la Maonesho ya Nanenane Mkoani Morogoro katika Manispaa ya Morogoro kwa awamu ya kwanza.

Halmashauri ya wilaya ya Bumbuli inapenda kualika Kampuni, Ushirika, Taasisi za serikali au vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria, wenye nia na uwezo wa kujenga Jenngo la maonesho ya Nanenane-Morogoro awamu ya kwanza kutuma maombi ya kazi hiyo bila kukosa.

SIFA ZA MWOMBAJI


1. MWOMBAJI AWE NA CHETI CHA UJENZI DARAJA LA SITA [Class six] AU ZAIDI.
2. MWOMBAJI AWE NA UZOEFU WA UJENZI WA MAJENGO MAKUBWA YA SERIKALI [AONYESHE KIAMBATA-BARUA/MKATABA ALIOPEWA NA MWAJIRI WA KAZI YA UJENZI KWENYE TAASISI YA SERIKALI]
3. MWOMBAJI AWE NA UWEZO WA KUSOMA MICHORO YA JENGO KUIELEWA NA KUITAFSIRI
4. MWOMBAJI AWE NA UWEZO WA KUJIRI MAFUNDI WASIOPUNGUA KUMI [10] AWE NA UWEZO WA KUWALIPA BILA USUMBUFU

Masharti ya kazi za ufundi

1. Fundi mjenzi anatakiwa kufika ofisi ya Afisa Manunuzi wa Halmashauri ya wilaya ya Bumbuli kwa ajili ya

kuchukua ramani na kujaza na *Schedule of labour Form* ya kuombea kazi za ujenzi.

2. Fundi Mjenzi Atatakiwa kujaza bei za kazi zote kwa kila hatua na kuweka viambatisho vyote husika
3. Fundi Mjenzi lazima afike eneo la Ujenzi ili kujirishisha na kazi kabla ya kuweka bei katika form atakayopewa.
4. Hakuna malipo ya awali (advance payment)
5. Malipo yatafanyika baada ya kufanya tathmini (evaluation) na kutolewa hati ya malipo (Interim payment certificate) iliyoidhinishwa na mtaalamu wa Ujenzi toka Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli
6. Malipo yote ya Fundi Mjenzi yatakatwa asilimia tano (5%) kwa ajili ya uangalizi (retention money)
7. Fundi Mjenzi atapaswa kuandaa mpango kazi kulingana na kazi zilivyoanishwa katika form ya kuombea kazi
8. Malipo yatakatwa makato yote ya kisheria yaani;
 - a. Kodi ya zuio asilimia tano (5% withholding tax)
 - b. Ushuru wa huduma (0.3% service levy)
9. Kazi zote zitasimamiwa na timu ya usimamizi wa mradi kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli ambaye atakagua, kufanya tathmini na kuidhinisha malipo yote.
10. Halmashauri ya wilaya ya Bumbuli haitalazimika kukubali maombi ya gharama ya chini ikiwa vigezo vingine havitafikiwa
11. Mwisho wa kupokea maombi ni saa 04:30 asubuhi ya Machi 07, 2023 (Jumanne) na kufunguliwa siku hiyo hiyo
12. Maombi yote yatumwe kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni, Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli, 02 Kitongoji cha Ugunga, 21783 Bumbuli. Lushoto, S. L. P. 111, Bumbuli.
13. Kwa maswali na mawasiliano yoyote tafadhali piga +255 653 192625



George D. Haule
Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya wilaya ya Bumbuli.

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
BUMBULI DISTRICT COUNCIL